

**MWAKA 2022 UWE NI MWAKA WA**  
**BWANA KUWAPIGANIA WATU WAKE HADI**  
**ADUI ATAMBUE HIVYO**  
**MAANDIKO: KUT. 14:10-14, 25.**

1. Wamisri wakasema “Na tukimbie mbele ya Israel kwa kuwa Bwana anawapigania kinyume cha Wamisri (**The Egyptians said “ Let us flee from the face of Israel, for the Lord fights for them against the Egyptians”**)

Kwa miaka mingi nimewaambia juu ya Bwana jinsi anavyowapigania watu wake na kuwaokoa na mambo mengi yaliyokuwa na malengo mabaya dhidi yao; na adui bado hakukata tamaa kuwafuatia watu wa Mungu mwaka hadi waka, mwezi hadi mwezi, wiki hadi wiki, siku hadi siku kama alivyokuwa akifanya kwa wana wa Israel

- **Lakini mwaka 2022 utakuwa ni mwaka ambao Bwana atawapigania watu wake hadi adui mwenyewe atambue na kisha akiri kwamba “aliye na nguvu kuliko sisi yaani Mungu Mkuu aliyeziumba Mbingu na Nchi na aliye na uwezo wote juu ya vitu vyote vilivyoko juu Mbinguni na vilivyoko duniani na hata vilivyoko chini ya Mbingu hii ndiye anayewapigania watu wake, na akiri kwamba Mungu yuko kinyume naye kabisa; na wateule tutatambua kwamba Mungu ni Baba yetu ambaye yuko upande wetu wakati wote.**
- Ni mwaka ambao Wateule tutaiona kazi ambayo Yesu aliifanya pale msalabani na ambayo anaendelea kuifanya hata leo katikati ya watoto wake kinyume cha adui zao; na viwango vya watu (wateule) kumcha Mungu, kumwamini (Kumtegemea) pamoja na kuwaamini watumishi wa Mungu wa kweli vitaongezeka. **Kut 14:31 ni lazima tena kabisa 2022 Watanzania wataiona kazi kubwa ambayo Bwana ataifanya!!**

- Siyo kwamba Mungu amekuwa hawezi kumshughulikia adui yetu muda wote ambao tumekuwa tukimwita na kumlilia katika dhiki nyingi tunazopitia, la hasha; uwezo anao na nia anayo; bali Bwana ni wa mipango, na wakati mwingine ananyamaza hadi akili zetu na uwezo wetu ufike mwisho ndipo ainuke na kutenda. **Mark. 4: 35 – 41.**
- Mwaka 2022 ni mwaka wa Bwana **kuinuka** na kutenda mwenyewe, maana akili zetu zimefika mwisho kabisa kuhusu hali ya hewa, magonjwa, uchumi, amani duniani manabii wa uongo, tauni mbali mbali; mvua nk. Bwana atatenda mambo makuu ambayo **yatamduwaza** ibilisi na kumwacha midomo wazi hadi akiri kwamba Mungu anawapigania watu wake Tanzania kinyume chetu!!
- **Natamani sana mwaka 2022 kila mwana wa Mungu halisi apokee ufunuo huu wa kweli juu ya ukuu wa Mungu tuliyemwamini na jinsi alivyo na uwezo mkubwa sana wa kumhukumu adui yetu ibilisi na kubadilisha historia yetu hadi adui mwenyewe akiri kwamba hawa hatuwawezi!!.** **Est.5:9-14, 6:1-14\*(13).**
- **Est.6:13:** Lazima kambi ya adui ikiri yenyewe **2022** hivi **“Ikiwa huyu Mwizarubi ameokoka na ametakaswa kabisa kwa damu ya Yesu, sisi kamwe hatutamweza; bali kuanguka mbele yake tutaanguka tu!! Then his wise men and Zeresh his wife said to Haman “if Mordecai before whom you have BEGUN to fall is of the off spring of the Jews, you cannot prevail against him, but you shall surely fall before him.**
- Huu ni ukiri wa hali ya juu sana wa kambi ya adui baada ya kupigo kikubwa toka kwa Bwana dhidi ya ibilisi na hivi ndivyo itakavyotokea **2022**, adui atapigwa hadi kambi yake itachanganyikiwa kabisa na itainua mikono dhidi ya wana wa Mungu halisi. **2Nyak 20:1-4, 14-17, 20-30\* 29-30**

- **Huu mwaka 2022 siyo mwaka wa kusoma historia za Mfalme Yehoshafati au wana wa Yuda (Israel) au Daudi, au Mordekai, au Daniel na kuona jinsi Bwana alivyowapigania; ni mwaka halisi wa Bwana kutupigania wateule wake wa sasa, ni mwaka wa Mataifa (adui) kutambua na kukiri kwamba kwa Watanzania yupo Yesu Kristo aliye hai ambaye anapigana vita vyao dhidi yao. Bwana amekusudia kutustarehesha kabisa wateule wake dhidi ya mapito na mashambulizi ya adui yasiyokoma mwaka hadi mwaka ambayo tumekuwa tukikabiliana nayo usiku na mchana**
- **Mwisho** - Hakuna sababu ya mteule yeyote kutahayari tena mwaka 2022 maadamu mkono wa kuume wa Mungu Baba uko pamoja nasi. **2Nyak. 32:7-8 na Zab. 118:15-17**  
“Miaka ya nyuma tumekuwa ni watu wa kusimuliwa matendo makuu ya ndugu zetu Waisrael pamoja na wengine kama nilivyosema hapo juu, **Mwaka 2022** ni mwaka ambao mbali ya sisi kusimulia matendo makuu ya Mungu wetu kwetu sisi wenyewe; Hata adui naye **atakiri** na kutambua kwamba Bwana yuko pamoja nasi na ndiye anayetupigania kinyume chake na kwa vyovyote vile hatatuweza kabisa. **Amina**

**Nawatakia baraka tele 2022 na mkono wa kuume wa Mungu Baba uwe pamoja nanyi nyote mwaka mzima ukitenda mambo makuu kwenu nyote kwa ajili ya utukufu wa Mungu Baba. Amina.**

**Na**

**Askofu Dr. L. M. Mwizarubi**

**1/1/2022**